Mlolongo wa kanuni katika maisha ya kiroho

( 0\12)

**Kristo anawapenda wenye dhambi ( 1)**

Usimamizi :
Nyumba ya Upendo wa Mungu

**Jina la kitabu** : Mlolongo wa kanuni katika maisha ya kiroho

( 0\12) Kristo anawapenda wenye dhambi

**Usimamizi** : watumishi wa nyumba ya upendo wa Mungu kwa wanafunzi

**Namba ya uchapichaji :** 455\2016

**Idadi ya kimataifa** : 9_805_30_9779_978 I.S.B.N

**Tuna matumaini katika Kristo kwamba ujumbe huu uwafikie vijana wakristo wote kwa bei rahisi sana .**
*** unaweza kutushiriki matumaini hayo kwa kuupa ujumbe huu kwa marafiki zako na wapenzi wako .**

**Ujumbe muhimu** : kwa faida kamili kutoka mlolongo huu , tafadhali usome kwa utaratibu sehemu kikamilifu kwani kutopanga husababisha mkanganyiko na kutoendelea husababisha kukata tamaa .



Utakatifu wa Askafu Tawadros ||
Baba wa Alexandria na Askafu wa Mtakatifu Marko ( 118)

## Utangulizi

Kristo anawapenda wenye dhambi , neno zuri na lenye utendaji wa ajabu katika kila moyo kwani sote ni wenye dhambi , iliandikwa kwamba wote wamepotoka wameoza wote pia , inamaanisha sote tumeoza lakini licha ya kuoza sisi tunapendwa na kukubalika kwa Mungu kwani Mungu anatuangalia kama wanawe ambao ni wagonjwa na wanahitaji matibabu , siyo kama adui wanaostahili kuadhibishwa .

Sehemu hizi zinazingatiwa kama utangulizi na maandalizi kwa njia ,tuzingatie na kumjua mungu na mtazamo wake kwetu kupitia kwa sehemu hizo , na kwani sisi ni wenye dhambi tutazingatia na mtazamo wake kwetu , sisi wenye dhambi , na jinsi anavyotendea nasi . kama ukitaka kujua upendo wa kristo na kukubali kwake na kubadilisha kwake , tunakuomba uendelee nasi ujumbe huo .

Mlolongo huu ni somo dogo pia ni hatua za vitendo katika maisha ya kiroho .

Bwana Yesu atupe kubadilisha akili na kukubali upendo wake kwa maombi ya Meryamu Bikira na Baba Tawadros || , na Utakatifu una Mungu kanisani kwake kwa milele , Amina .

Nilitembea njiani  kuelekea Baba yangu , mimi na kaka mmoja ambaye alipenda pia kuanza masomo ya kiroho nimeyoyaanza . Tangu nimeanza maisha ya kiroho nilijifunza mengi , wakati niliosubiri tokea zamani umeshakuja niwaambie wengine kuhusu masomo hayo na wanaanzaje uhusiano na Kristo , na kwani mimi niko mwanzoni mwa kazi , kwa hivyo kile naweza kuchofanya ni kuwasaidia wanaotaka kurejea kwa Baba yangu na yeye atakamilisha nao , Baba yangu ameniambia kwamba baada ya muda fulani naweza kuanza nao pia .

Ama kuhusu rafiki yangu , ni mtu mwema sana na mpole sana lakini kwa matukio yaliyotokea kwake zamani na kwa athari ya mazingira , akabadilika kabisa , akawa mkali sana kisha akaanza ulevi , akaendelea katika nijia ya dhambi na hatia , na hii siyo lawama  lakini ilitambulika na marafiki zake , yaani wanajua hivyo , mpaka achaliwe na kanisa na watumishi kwa umaarufu wake mbaya , lakini ukikaa naye , utaona nadani yake mtoto mpole ana hamu sana ya kurejea kwa kristo na kwa maisha mazuri , lakini vipi ? wote wanamwacha na hamna anayemvumilia .

Kwa mfano maneno yake haiwezekani kubadilika ghafla , na mambo ambayo alizoea kuyafanya zamani hawezi kuyaacha mnamo sekondi , kwani yeye ameshajaribu hayo yote mara nyingi bila faida , akisikiliza tu “ umeshaokolewa , wewe sasa ni mtu mpya”, lakini baada ya siku chache , anayafanya tena mambo mabaya haya , alikuwa akikata tamaa na kujiambia : “hamna faidia “ , na njia hii siyo yake , pia alikuwa anasema mara nyingine kwamba wanaotembea njiani hiyo sio wenye haki  , kwani hamna maabadiliko wala kitu chochote , hao wanaishi hivyohivyo , kanisani wawe watumishi na wenye kuonya , na njeni wanaishi bila uhakiki kwa maneno yaleyale yenye vikwazo na mabaya .

Alijaribu kuhuduria vikao vya kanisa , akasikia kwamb toba ya kweli ni kutorejea kwa dhambi tena . akajaribu na kujitahidi kwa nguvu mara kadhaa , lakini katika kila mara alikuwa anashindwa kwa dhambi hizohizo , akakata tamaa , “ ikiwa toba isiyo kweli kwa nini niache dhambi ? “ , lakini wakati alipojua kwamba toba ni njia kamili siyo hatua tu , akajipa moyo , na nilipomwambia kuhusu Baba yangu , akahamisishwa aje kwake ili kukamilisha njia naye , ambayo nimeianza tokea miezi .

Tulitembea pamoja tukisimulia upendo wa kriso kwa watu wenye dhambi , mara tulifikia , tukampata Baba akitusubiri , akatupokea, tukaketi , nikamtambulisha rafiki yangu , nikaomba kuondoka niwaache peke yao .

Wakati rafiki yangu aliponiacha pamoja na Baba nimejisikia haya sana , kwani sura yangu ya nje na nywele zangu ndefu inawakasirisha baba wengi na watumishi katika kanisa langu , lakini hii ni asili yangu , mimi napenda hiyo , ninajiambia wakati wote " je , Mungu anajali nyewele ndefu au fupi ?"

Nilijisikia haya ingawa ushujaa wangu katika mambo mengi ila wakati napoongea kuhusu Mungu na mambo ya kiroho , najisikia haya sana .

Baba akanishangaza na upole wake na tabasambu lake zaidi ya hayo alinishangaza na kukubali kwake bila ya kutoka maoni . kwani kitu nakichukia zaidi ni kujua maisha yangu binafsi , wanaokutana nami wananiuliza " mbona nyewele zako ni ndefu ?" Ee mzee ni nywele zangu au zako ! siyo kazi yako kabisa " lakini Baba huyu ni mwiongoni mwa wachache amabao hawaniulizi kuhusu nyewele zangu , bali nikajisikia naye kama yeye ananijua tokea muda , akanisalimia akisema : vipi mwanangu ?"
nikasema : namshukuru Mungu , Baba

Akasema : mambo yanaendeleaje ?
nikajibu : kama rafiki yangu alivyokwambia kwamba mimi niko mbali sana na Mungu na nimefanya mambo mengi haifai kuyazungumzia , na unaweza kusema nimependa hatia sanasana , hatia zote . nikajaribu sana kutubu na kurejea kwa Mungu lakini nikashindwa .

Lakini nilisoma kitabu " vipi nianze " nikajipa moyo nilipojua kuwa maisha ya kiroho ni njia na siyo hatua , nikahisi kuna matumaini hata madogo baada ya kukata tamaa na kutomwamini Mungu ama kujaribu kujiua , yaani sijui !! laini nimechoka sana, zaidi nimevunjika , nilipojua ni afdhali niwe na mtu anayenisaidia njiani , kaja kwako Babangu hasa nilipomwona rafiki yangu abadilike kwa kweli , na nikaona upendo wa kweli kutoka kwake na kujali binafsi siyo kujali kama kawaida na kwa sura tu , vilevile hatua za vitendo nilizozisoma , zinarahisisha njia .

Akasema : sawa mwanangu , pamoja na hatua za kiroho ulizozisoma katika “ vipi nianze “ , ambazo tutazirudia pamoja tena , tutazungumzia kwanza mfululizo mwepesi unaitwa “ Kristo anawapenda wenye dhambi “ . lazima tuweke misingi kabla ya kuanza .

Nikasema : jina la kitabu ni zuri babangu , pia nimeshaongea na rafiki yangu kuhusu jambo hili , bila shaka alijifunza mengi kutoka kwako , Baba yangu , lakini dalili gani inayothibitisha kwamba kristo anawapenda wenye dhambi ?

Akaema : **zipo dalili tatu kuhusu upendo wa kristo kwa wenye dhambi**

**Dalili ya kwanza ni maneno ya Biblia Takatifu**

Niksema : tafadhali usimulie kwa upole kwani mimi siye mtu wa kanisa , sijasoma Injili kabla ila mara chache , pia sijui kanuni za kanisa na nikihudhuria kikao na wakiimba kwa lugha ya kikoptiki nitajisikia kama nipo China . kwa hivyo uanze nami kama mtoto katika mambo ya kiroho .

Akasema : kristo anawapenda watoto , yeye alisema :
“ Waacheni watoto wadogo waje kwangu , wala msiwazuie ,
kwa kuwa watu kama hao ufalme wa Mungu ni wao “ ( Luka 18:16 ) .

Ama kuhusu upendo wake kwa wenye dhambi Yesu alisema :
“ Wenye afya hawahitaji tabibu , bali walio hawawezi ,
sikuja kuwaita wenye haki , bali wenye dhambi “ ( Marko 2:17 ) .
wakamzungumzia “rafiki yao watoza na ushuru na wenye dhambi ! “ (Mathayo 11:19) , pia “ Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee , ili kila mtu amwaminiye asipotee , bali awe na uzima wa milele “ ( Yohana 3: 16 ) .

Vilevile Mungu anasema katika kitabu cha Nabii Isaya : “ Haya , njoni , tusemezane . asema BWANA . Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana , zitakuwa nyeupe kama theluji ; zijapokuwa nyekundu kama bendera , zitakuwa kama sufu “

Afdhali kwa binadamu ajue thamani yake amabayo ni muhimu sana kwa Mungu na kwa wana wa mbingu , afahamu upendo wa Mungu amabaye alimtoa Mwanawe pekee , ili kuipa nafsi yake uzuri wake kwa damu yake yeneye thamani ....
Mar Yakubu EL Sorogy ...( upendo wa kimungu , ukurasa 57)

Nikasema : ni nini Bandera , Babangu ?
Akajibu : Bendera ni rangi nyekundu , yaani nyekundu sana , pia nyekundu ni kama dudu mwekundu , inamaanisha kuwa kama hatia zenu ni za kidamu na mbaya sana , njoni kwangu nizifanye ziwe nyeupe kama theluji na sufu .
Niksema : habari njema . inaonekana sikuishi !!

Akasema : hatungeamini maneno ya Mungu kuwa anatupenda na kutujali na kutukabili bila ya kuona hatia zetu , tutapotea. Kwani yeye anawapenda wenye dhambi , na yeye atazifuta dhambi na kusamehe ( Isaya 55:7 ) . lakini Shetani ana lengo la msingi ambalo ni kuharibifu mahusiano yetu baina ya Mungu . akatupa mawazo kama kuwa Mungu ameshachoka na kutupinga kwa ajili ya uwingi wa hatia zetu . " lakini yeye ni mwongo na baba wa huo " ( Yohana 8 :44 ) .

Nikasema : lakini kwakweli naanguka sana na hatia zangu ni mbaya !!

Akanijibu : kuna neno , mwanangu ,lenye uharibifu tunalisema sana bila ya kujua kwamba linasababisha uharibifu kwa uhusiano wetu na Mungu , na sisi tunadhani ni unyonge .

Nikasema nikistaajabi : neno gani , Babangu !
Aksema : unaposema ( namhuzunisha Mungu )

Niksema kwa nguvu : nafanya dhambi nyingi , kwa hivyo namhuzunisha Mungu , si ndiyo !

Akasema : unapenda kuzifanya hatia hizo ?

Nikajibu : hapana , nataka kuziacha , nani aniokoe !

Akasema : kwa hivyo wewe humkasirishi Mungu , Mungu anakwambia , Shetani anatukasirisha mimi na wewe . kama mtoto mdogo anatembea njiani na mtu mbovu akamtupia takataka , je, babake atakuwa na huzuni kwa sababu yake ama kwa sababu ya yule mwingine ? !

Nikasema : kweli , kwa sababu ya mtu mbaya .

Akasema : sisi pia tunapofanya dhambi , lazima turudi kasi na tujue kwamba Mungu anatukubali , anatuosha na anatukumbatia. Lakini neno la Mungu ana

huzuni Kwa ajili yangu ni neno kutoka shetani ili mtu asirejee kwa baba yake na abaki kumuogopa Mungu na asimame bila kusubiri msaada bali adhabu, na atabaki kufanya dhambi !! Au anajaribu kumridhisha babake mgumu huyu ambaye hamsikii , labda amkubali na mara kwa mara kurudi kunakuwa jambo gumu sana kisha atakata tamaa na atasema : "Mungu amechoka kwangu" na hapa shetani anacheka Kicheko cha kishetani

"Ha , Ha , umeanguka mkononi mwangu , Sitakuonea huruma "

Nikasema : Eeh , kweli ni neno la kishetani na lenye uharibifu , sikuelewa ujanja na hila za shetani.

Akasema : kuna kijiji kikubwa lakini idadi ya wakristo ni ndogo sana na vijiji kama havyo vinahitaji Utunzaji maalumu wa watumishi na kanisa kwani kutokuwepo kwa kanisa ndani ya kijiji au karibu yake na Huduma isiyo ya kawaida kunafanya utamaduni wa watu rahisi uwe mbali na injili na kristo na wawe mawindo mepesi kwa shetani . Kijana alisafiri kwa yordani ili kufanya kazi pale na aliacha mke wake aliyemwoa tangu miaka miwili pamoja na mtoto wao mdogo , aliahidi kumtuma barua kila mwezi na pesa ili anazitumia na kwa sababu yeye hajui kusoma , alimshauri aende kwa familia yake ili kuisoma barua na kutumia pesa kwake kisha baadaye alimtuma barua kwake kila mwezi nayo agizo la pesa naye akawa alikwenda kwa familia yake ili kusoma barua na kutumia pesa , lakini kwa sababu ya kijiji yake ni mbali kisha akawa mvivu na alikwenda kwa mojawapo wa jirani na alimwomba kutumia pesa kisha alitumia pesa kwake , kisha mwezi baada ya mwezi alimwomba kusoma barua kisha akaanza kufanya hivyo na ili asije posta , aliamuru kuoa barua na pesa kwa mtu huyu na kila mwezi husoma barua na humpa pesa .

Na katika siku fulani , mtoto akawa mgonjwa na kwa sababu ya elimu yake rahisi , hakumtunza vizuri na maradhi yalizidi , na

Jirani akachukua fursa hii na wakati alisoma barua na Akakumwambia uongo na

amenukuliwa kutoka ulimi wa mume wake kwamba yeye alisikia juu ya ugonjwa wa mtoto na kusijali kwake na ataadhibiwa vikali . Mwanamke aliogopa na

aliamini maneno ya uongo na mtu huyu alianza anazungumza maneno mabaya na alisema

Usiogope , nitakuwa nawe na siku baada ya siku , anamuogopa kutoka kwa mume wake kupitia barua za bandia na maneno ya uongo

Na kutoka upande mwingine alisema maneno ya upendo na unafiki . Na kutokana na hofu nyingi , aliacha kristo na alimwoa . Kisha mume alikuja baada ya miaka miwili na alimwona barabarani na alipiga kelele kwake " Hatuna uhusiano kati wetu , ikiwa anazungumza , nitamwabia polisi " . Mume alishangaza sana na akasema "nini , unasema nini ?" Alisema : "wewe si mume wangu na sikujui " lakini mke alishtuka kuwa kile alichodhani katika barua , kulikuwa uongo "

**Na hivyo wewe** pia ikiwa haukubali maneno ya yesu kwako na upendo wake wazi kwako

Katika biblia takatifu , ikiwa ulisikia maneno ya uongo kwamba umemhuzunisha Mungu , naye amechoka na wewe na atakutesa na kwamba hakuna matumaini , fursa ilipotea , na Toba ni bandia , wokovu ulikuja katika sekunde na ikiwa tunarejea , tutakuwa wasiotubu na wakati ulipita na Hatuna wokovu!! Ni maneno bandia , si sahihi na si kweli , mwanangu . Hii inatufanya kukataa tamaa katika sisi wenyewe na katika kukabilika kwa Mungu kwetu .

Na lakini kristo anawapenda wenye dhambi wote , wazinifu , hakukataa mashoga , anafurahi kurudia kwa watu wasioamini kuwepo kwa Mungu bila ya kudhalilisha mtu , anapenda na anakubali bila ya sharti na hata hahitaji toba ili anakupenda , anakukomboa na anakusamehe .

Nikasema : pole pole , babangu , kwani sielewi vizuri , nini maana ya hahitaji toba kwa upendo au pia kwa ukombozi ?

Akasema : Mungu anatupenda ikiwa hatutubu ,

Anatupenda na sisi ni wenye dhambi , hajasema tubuni kisha nitakupenda , lakini kuna aya tunaiita siri ya mageuzi katika maisha ya kila mtu , Na anayekubali aya hii , maisha yake itabadilika kutoka kushindwa kwa ushindi , kutoka utumwa wa shetani kwa uhuru wa kristo na kutoka giza la dhambi kwa nuru ya uadilifu .

Nikasema : aya gani inajumuisha siri hii?

Akasema : ni katika barua ya mtume paulo

Warumi:5.8

"tulipokuwa tungali wenye dhambi." Yaani tungali wenye dhambi , hatutubu , haturudi na hatubadilika

" Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."

Yaani upendo wa Mungu ilionyesha bila sharti , upendo wake hauweka vikwazo juu yetu ili kuzidhihirisha na kweli ikiwa usikubali upendo wa Mungu wakati wa dhambi , hataturudi wala hatatubu kamwe .

Akasema : babangu , vipi ?

Nikasema : kristo alikuja ili anatuokoa kutoka dhambi kwani pekee yetu hatuwezi . Yeye ni daktari nasi ni wagonjwa , Tunamwendea ili kututibu .

( Na ghafla bila utangulizi wowote , babangu alishika tumbo wake na akilia ah ah ah )

Nikasema : nini , babangu ?

Alisema : ah , ah .

Nikasema : ( kwa hofu ) : twende hospitalini

Kwa haraka .

Akisema : ah , ah .

Nikasema : twende kwa haraka , babangu .

Alisema : tutakwenda , tutakwenda lakini sio sasa . Ah , ah .

Nikasema : kwa haraka , babangu .

Akasema : nitakwenda , lakini baada ya kupona kwangu .

Mungu anakupenda , anakupenda na anakupenda nawe katika Undani wa dhambi , anakupenda , anakupenda katika wakati wa

Kumtukana Mungu na kumkana , anakupenda licha ya chuki yako na anakutaka mwana wake , anakuokoa kutoka kwa mtego na ufisadi wa asili yako .......

Mwenye athari origanos , upendo wa Mungu ,

(Baba tadrous yacoub malti ) ukurasa wa 365

Na wakati dhambi ilipozidi , neema pia itakuwa nyingi zaidi

( Liturujia ya kimungu )

Nikasema : kwa haraka , babangu?!

Na hapa babangu alicheka na alisema baada ya kupona kwangu ,
nitakwenda kwa daktari ( ulifahamu mfano )

Nikasemo ( kwa tabasamu ) : Aliniogopa , babangu ,
lakini ni mfano wazi ( lakini ninatamani ungeniambia mapema ili nisiogope )

Akasema : haina maana kwamba napona kisha nitakwenda kwa daktari , kwani ninakwenda kwa daktari kwa ajili ya ugonjwa wangu .

Nakadhalika haina maana kuwa Nitakuwa huru na dhambi na baadaye nakwenda kwa kristo na atakubali upendo wake .

(Warumi:5.20)

na dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi

Nikasema: nami mwenye dhambi na anafanya dhambi kubwa sana na Mungu ananipenda.

Nikasema : naam , wakati nilipokuwa nikifanya dhambi nyingi , Mungu ananipenda zaidi kama ilivyoandikwa katika

( Warumi:5.20) "dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi"

Nikasema : maneno mapya na yenye ajabu , vipi ?

Akasema : daktari wa mifupa ana watoto watano , mtoto mmoja alikuwa amecheza na mpira , Alikuwa na mguu uliovunjika , babake akimpelekea hospitalini na alitibu miguu yake

, Atajali nani zaidi ?

Nikasema : kweli , mwenye miguu iliyovunjika .

Akasema : na baada ya siku tatu , mtoto mwingine alishuka ngazi na alianguka kisha alivunjika , atajali nani zaidi ??

Nikasema :kweli , aliyevunjika

Akasema : na baada ya wiki , mtoto wake mdogo kabisa alijeruhiwa katika ajali na uti wake wa mgongo ulivunjika , unadhani atajali nani zaidi ? Atajali watoto wema au mwenye miguu iliyovunjika au wa mwisho ?

Nikasema : wa mwisho , kwani hali yake

Ni ngumu sana .

Akasema : na kadhalika , Mungu anawapenda wenye dhambi na anawajali , kama yesu alivyotaja katika mfano wa kondoo aliyepotea

Kwamba yeye aliacha kondoo 99 na alimjali kondoo huyu , kwani anamuhitaji bali yupo katika haja kubwa zaidi lakini shetani anasema uongo : (Yohana:8.44)

(kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo.)

Mungu anachoka kwako , naye anawapenda

Watakatifu , ama wewe anakuandaa kuzimu .

Na binadamu ni maskini , anajaribu kujitibu na kujiokoa mwenyewe na kwa sababu Mungu anakuandaa kuzimu na bila ya ufahamu wa binadamu , anahisi kumuogopa Mungu bali inaweza Anachukia na anamkataa Mungu.

Wakati alipoanguka , kabla ya kitu chochote ,

Usijilaumu mwenyewe na anasema

Je! Hii ilitokeaje kwangu ? Ni kilio ! Bali uwe mnyenyekevu na Inua macho yako kwa Mungu na sema kwa moyo yako yote : Mungu , kitu kipi kinatarajiwa kutoka mtu dhaifu na mwenye dhambi kama mimi ili hiki

Na umshukuru baada ya hayo kuwa jambo halikudumu zaidi , ukisema : Mungu , bila ya Rehema yako isiyo na mipaka , Singekuwa nimeacha hapo lakini ningeanguka katika mambo mabaya zaidi

B/ Thiofan ( sehemu ya pili , UK 86)

Kuna mtoto katika Daraja la tatu la msingi , alikuwa amecheza katika Shule za Jumapili (kanisani ) na mwalimu aliyekuwa amechezea darasani alisema kuwa Mungu atampelekea kuzimu , mtoto alirudi nyumbani na aliingia jikoni na alikuwa naye picha ya kristo kisha aliiweka kwenye jiko na aliichoma na mamake aliingia na alipiga kelele usoni mwa mtoto "unafanya nini , mtoto wangu " , alisema " nimemchoma kabla ya ananichoma " , alisema " unasema nini " , akajibu : "kwani katika kanisa , walimwambia

Kuwa yesu kristo atampelekea kuzimu , kwa hiyo nilisema nimchome kabla ya ananichoma "

Ni bora kujuta kutoka undani wa moyo wako , lakini licha ya undani wa juta ,

Usiruhusu Kufanya uwe mtuhumiwa katika msamaha , kwani msamaha uliandaliwa kabla kikamilifu , Vyombo vyote vya dhambi vilibomolewa msalabani

B/theifan ( sehemu ya pili , UK 86)

Nikasema : eeeh , kwa kiwango hiki!!

Akasema : ndiyo , mwanangu , ikiwa hatukubali upendo wa Mungu kwetu nasi wapo katika undani wa dhambi kama biblia ilivyosema , tutamkataa Mungu bila ya ufahamu na tutamchukia , nayo inavyotokea na wasioamini katika uwepo wa Mungu , kama mtakatifu Augustine alisema : "Nyuma ya kila kutokuwepo kwa Mungu ni tamaa"

Na kwani yeye anadhani kwamba Mungu anamchukia kwa sababu ya tamaa na dhambi yake , kisha akaanza yeye mwenyewe

Anamchukia na anamkataa .

Lakini ikiwa anakubali kuwa Mungu anampenda naye akifanya dhambi , hii itakuwa kuanzia kwa mageuzi yake .

Nikasema: maana yake kuwa mwanadamu abaki katika dhambi na tamaa zake, na aseme kuwa Mungu bado ananipenda?!!

Akasema: baba amependa mtoto wake ambaye alijeruhiwa katika ajali, mgongo wake ulivunjika na nyonga yake ilivunjika, lakini hapendi kuvunjika na ugonjwa, Mungu anapenda mwenye dhambi, lakini hapendi awe katika dhambi.

Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa

Uwaagize wasijivune, wala

Wasiutumainie utajiri usio yakini, bali

Watumaini mungu atupaye vitu vyote

Kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha.

(1timotheo 6:17)

Mungu ni daktari wa nafsi mwenye ujuzi, anajivunia wagonjwa wake, bila kujali ugonjwa wao ni mbaya, sio upendo katika magonjwa, lakini ili kuokoa wagonjwa wake kutoka kwa uzito wa ugonjwa.
Alama ya Origanos_ upendo wa kimungu _ukurasa 365

Dhambi kama nikikwenda barabarani na shetani akanipiga kichwani mwanangu nikarudi kwa baba ili kunisukuma na kunitia moyo na kuniambia "usiogope, wewe ni mpenzi wangu na nitamwonesha", lakini mtu akienda kwa shetani na kumwambia, nipige shetani ili Mungu aniguse kwa upendo, utamwambia nini ?!

Nikasema: kweli ana wazimu, nisamehe, labda huu ni ujinga?!

Akasema: Mungu anatupenda wakati shetani anapotukosea, dhambi ni uchovu, majeraha, hatia na hofu, tunahitaji upendo wa Yesu, kumbatia, uhakikisho na kupona kwake, lakini hakuna mtu mwerevu anayesema kwamba mimi ni mgonjwa na Mungu atanigusa kwa upendo.

Nikasema: sawa Baba, umenielezea hatua muhimu sana, lakini umeniambia kwamba toba sio sharti la upendo, na sio sharti la msamaha, nilielewa kuwa Mungu ananipenda, nikitubu au singetubu , na sababu ya kurudi ni kwamba Mungu ananipenda, kwa hivyo narudi kwake, lakini inamaanisha nini kwamba toba sio sharti la msamaha, inamaanisha kuwa Mungu anaweza kunisamehe na mimi sijatubu ?

Akasema:

**Toba sio sharti la msamaha**

**Bali**

**Ni njia ya kukubali msamaha**

Nikasema: samahani, uwezo wangu wa kuelewa ni dhaifu, sikuelewa sehemu hii.

Akasema: mwana mpotevu, alikuwa pamoja na nguruwe na akiishi na wazinzi, alitumia pesa za baba yake katika ufisadi, lakini baba yake alimpenda na kumngojea, kila asubuhi, alikuwa akiangalia barabarani, akitumaini kwamba mtoto wake arudi, basi mwana alikuwa na nguruwe na alikuwa na dhambi, lakini baba alikuwa anamsamehe dhambi zote na moyo wake ulikuwa umejaa upendo kwa mtoto wake.

Toba tu ndiyo njia ambayo mwana huchukua ili asamehewe,

**Toba haikuwa sharti, lakini njia**

Msamaha ulikuwepo kabla mtoto hajarudi, lakini hangekuchukua njia ya kurudi (toba) hatapokea msamaha na kuchukua, licha ya uwepo wake, na imeandikwa unirudie; maana nimekukomboa (Isaya 44:22) sio nitakukomboa, ninarudi kwa sababu Mungu alinikomboa na akarudi kuchukua ukombozi.

Nikasema: nimeelewa baba yangu, kuwa Mungu amekuwa akinisamehe kila wakati na toba sio sharti la msamaha wangu lakini ni njia ya kurudi kukubali msamaha, sikirudi, sitasamehewa na nitakufa licha ya uwepo wake.

**Nimeyafuta makosa yako kama wingu zito, na dhambi zako kama wingu; unirudie; maana nimekukomboa. (isaya 44:22)**

Na lakini nataka kukuliza, unasema kuwa Mungu hataki kumwangamiza mtu, lakini mtu aliye na hiari yake ya kuchagua ndiye anamkataa Mungu (uzima) na Kumwatengwa naye (kifo), sawa, sitaki hiari yangu Kwa sababu najielewa kuwa ninataka ubaya na Unajisi tu. Mambo yangu ya ndani yalikuwa yamejaa ubaya, na unajisi ulinitawala.

Sitaki hiara yangu, ninataka Mungu aniongoze barabarani

Hata ikiwa siyo ni mapenzi yangu!!

Akasema: kwa kweli hii ni toba, mwanan!

Huu ni mwanzo sahihi wa maisha yako ya kiroho, na umeshauanza. Hii ni hatua ngumu sana ni kukubali ufisadi wako na dhambi na usikiburi au kuhalalisha, lakini kukubali kunapeana mapenzi yako na uhuru wako kamili kwa Mungu, unaliamini neno la Mungu, alisema "wote anipao baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe" (Yohana 6:37). ukipeana hiari yako na maisha

yako kwake, ndiye anayewajibika kwako na atakutunza, yeye ni " awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu" (yuda 1:24).

Nikasema: je ! unamaanisha nini, baba? Maana yake kuwa sitafanya dhambi tena!

Akasema (akitabasamu): hii sio naimaanisha, lakini ninamaanisha kuwa wewe ni mgonjwa na ulijisalimisha mwenyewe kwa baba yako mwenye upendo ambaye pia ni daktari hodari, jukumu liko juu yake, kupona kwako ni jukumu lake . Lakini kupona hakutatokea kwa muda mfupi, lakini kutachukua wakati wake.

**Unapaswa kuzingatia matibabu (njia za neema)**

**Na ufuate maagizo ya daktari (Biblia takatifu)**

**Na uwe mbali na vyanzo vya maambukizi (njia mbaya)**

**Na ujikute bora siku kwa siku utakapopona**

**kikamilifu.**

Jambo linalokusaidia Zaidi ni ujasiri wako kwa daktari ambaye ni baba yako.

**Kwanz :imano yako katika upendo wake**

Tabasamu la daktari na maneno
jwa na ujasiri wako kwamba anakupenda na hatakudhuru, hatakuumiza na hatakwambia kwa nini wewe ni mgonjwa, wewe ni mjinga, mchafu na usistahili chochote.

**Pili: imani yako katika uwezo wake**

Hakikisha kabisa kuwa daktari yako anaweza kuponya magonjwa yako yote na kukufanya huru kwa dhambi yoyote.

Nikasema: kweli, je! Niitakuwa huru kabisa kutoka kwa dhambi zangu, tabia zangu na unajisi ?

Akasema: Biblia ilisema "tena itakuwa katika siku ile, ambayo bwana atakupa raha baada ya huzuni yako, na baada ya taabu yako, na baada ya utumishi ule mgumu uliotumikishwa". (Isaya 14:3)

Mungu alisema, kwa hakika itakuwa.

Nikasema: je! Siku hii itakuja katika maisha haya. Kwa maana itakuja siku ambayo nitakuwa bila dhambi, bila shida na tabia mbaya!!

Akasema: hili silo kusudi letu wala lengo letu, basi

Lengo letu ni ishara ya upendo

Ya kweli na Mungu.

Siku itakuja ambapo mwana atapona, atamka, atacheza na kufuraha na baba yake, lakini katika maisha yake yote, atabaki hatarini, lakini pia ikiwa yuko na baba yake, atabaki salama na akiumia hatamwacha, kwamba jukumu la uhifadhi wake na kupona ni jukumu la baba yake, na ni dhamani yake yote. (Waebrania 7:22)

Nikasema: maneno yako yanatia moyo na kunifariji baba yangu, na yanarudisha Imani kwangu kuwa nimependwa na kwamba kuna tumaini baada ya kukata tamaa na mashetni hupiga kilele masikioni mwangu, "hakuna tumaini wewe ni mkosaji mkosaji, wewe ni najisi najisi" hasa baada ya kuanza katika ujana na kuanza kuanguka katika tamaa, tabia za ujana na kuona vitu vibaya, unanielewa, Baba?!!!

Akasema: nakuelewa mwanangu, wewe si peke yako, mwanangu, lakini ni hali ya vijana wote wa kizazi chako na hii ni vita ya asili.

Nikasema (ninajisikia vizuri): kweli, Baba ?

Akasema: vijana wanapopambana na tamaa za ujana na tabia mbaya na kuanguka, shetani anapigana na kukata tamaa na wanajiangalia na dharau na kuwa wao ni najisi na wanafikiria kuwa Mungu aliwakataa n wanamkasirisha wanaposhindwa na shetani, lakini suala ni tofauti kabisa.

Nikasema (akiisumbua kama kwamba kuna mtu alielezea hali yangu kabisa): je ?!

Akasema (kwa utulivu na upendo kama daktari huponya majeraha kwa upendo wote na uangalifu): vita vya shetani ni vita vya majira.

Inamaanisha kuwa katika utoto tunapigana na matusi, kuapa na kusema uwongo kwamba tunajifunza kutoka mitaani au shuleni. Ujana ni vita vya tamaa, tabia na sura mbaya. Hatua baada ya kuhitimu na kufanya kazi ni vita vya kujali na vyenye shughuli nyingi. Na Shetani wa utoto ni shetani mdogo kama watoto, na shetani baada ya kuhitimu huanza uzee pamoja na kupita wakati, lakini shetani wa hatua ya ujana ni shetani kali na uchovu, kwa sababu vijana wana sifa ya vurugu, nguvu na hawapendi kushindwa, wanapoanguka katika dhambi, wanakasirika, wanapata hzuni na wanachukua suala hilo kibinafsi, je ! nitaangukaje ? (hata kama kijana huyo alivyoshindwa katika mchezo, akikasirika).

Nikasema: kweli, kama nikishindwa katika mchezo wowote, mimi nakasirika, na ikiwa mchezo uko kwenye komputa, ninataka kuivunja.

Akasema: lakini katika maisha ya kiroho, tunapambana na shetani. ukishindwa, amka haraka, usikate tamaa na ususikie sauti yake mbaya "wewe ni Haifa, wewe ni mkosaji mkosaji na najisi najisi".

Nikasema: na anapokuja kwangu na kuniambia hivi, nifanye nini, Baba?

Akasema: jibu na kumwambia

**Damu ya kristo ilinisafisha kutoka dhambi zote,**

**Damu ya kristo ilinisafisha kutoka dhambi zote .**

**Rudia hadi vita hivi vitakapomalizika**

Neno la Mungu ni upanga ambao umeutumia na kupingana na shetani, badala ya udhalishaji na kukuchosha. Unaamini kuwa unapendwa na kukubaliwa, na kwamba unaokolewa katika damu ya kristo, haijalishi umeanguka mara ngapi, hata ikiwa ilikuwa mara milioni kupitia siku moja, jambo muhimu ni usidhani ni rahisi n usiukate tamaa.

Nikasema: kweli, sauti hizi zilinifanya nikate tamaa na nilikuwa karibu niwe na wazimu. Tafadhali Baba, usiniache kabla hujakamilisha mtaala kwangu kama ulivyofanya na rafiki yangu.

Akasema: kristo hatawahi kutuacha.

Itakuja hatua kwa hatua. Je! Tunaombaje,

Tunawezaje kuachiliwa kutoka kwa

Maanguko ya mara kwa mara na

Tunaamini vipi ,kuna mambo

Mengi katika msamaha tutasema moja

Kwa moja na kwa neema ya kristo

Itakuja hatua kwa hatua.

Bwana wangu yesu, nina deni kwa aibu yako ambayo iliniokoana matendo yako ambayo yaliniumba, nini maana ya maisha bila Baraka za wokovu ?

Mtakatifu Ambrosyos

Nikasema: nataka mafunzo ya vitendo Baba yangu, rafiki yangu ameniambia kwamba kila wakati tunapojifunza mafunzo, ninapaswa kuyatumia maishani mwangu. Lakini ni bora kuwa hatua za vitendo zinafaa hali yangu rahisi, kama unavyoona , si ndiyo ?

Akasema: kweli, tutachukua mafunzo ya vitendo ili kuona matokeo. Na maneno yetu yatakuwa kwenye ngazi mbili, kiwango cha akili na kiwango cha vitendo. Kiwango cha akili ili kubadilisha mawazo ya zamani ambayo yalituathiri kutoka kwa jamii. Na kiwango cha vitendo ni matumizi ya vitendo. Samahani, kwanza tutazingatia juu ya kiwango cha akili na mafunzo rahisi. Kisha nitakuambia hatua za vitendo katika nukta tatu.

Nikasema: je ! ni hatua gani, Baba ?

Akasema: kwanza, soma Biblia takatifu.

Nikasema: baba, sijasoma katika Biblia tangu wakati nilipozaliwa labda mara moja au mara mbili ?!

Akasema: sawa, tutaanza na mwanzo rahisi kwako, soma aya moja kila siku.

Nikasema: aya moja tu.

Akasema: tafadhali mwanangu, nifuate hatua kwa hatua, ambayo ni aya moja kila siku kwa wiki, na aya mbili kwa wiki ya pili, na kipande kimoja kwa wiki ya tatu, na nusu mlango kwa wiki ya nne, kisha kamilisha njia hii kwa mwaka. Je! Unaweza kufanya hivyo ?

Nikasema: hii ni suala rahisi na nitasoma

Zaidi ya hii pia …..

Nguvu ya Biblia ni kwambe iwe maombi , na nguvu ya maombi ni uzitumie aya za Biblia Takatifu Biblia.

Akasema:tafadhali usiongeze , na ukisimamisha kusoma zaidi ya wiki mbili ,anza mara tena kotoka mara ya kwanza aya na aya ,mbili na kadhalika na mambo muhimu zaidi katika Bibla takatifu ubadilishe ahadi zake na manemo yake kwa sala .sio kusoma kwa kujua taarifa na Mungu akipenda tunajua zaidi wakati tunazungumza jinsi ya kusoma Bibla takatifu .

nikasema:kwa nini Baba yangu nimesikia kwamba rafiki yangu anasoma sura tatu na sala za agbia !?

akasema:rafiki yako ameanza kama hivyo na hatua kwa hatua alianza kukuza sio mara moja tu ,kwani kuzoea ni kanuni muhimu katika kwa ukuaji na mwendelezo,katika kiwangu cha kimwili au kiwangu cha kiroho .

nikasema:hizi kwa Bibla na nini Agabia ?

akasema:lini umesali mara ya mwisho ?

nikasema:sikumbuki mwaka au zaidi

Ukuaji hatua na hatua kutoka utoto mpaka ukuaji na ukamili katika kiresto kwa hivyo ngome za mawazo mabaya hupenguka hatua kwa hatua ala hupenguka kamili st. Macarius mkubwa

akasema :haya , dakika moja kwa kila siku kwa wiki moja
halafu dakika

mbili kwa wiki mbili ,thabitisha dakika tanu kwa miezi tatu

usiongeze wala usipunguke.

Nikasema : niombeje ?

akasema omba kwa mahitaji yako (vitu vitatu : mambo ya kiroho , mambo ya kimwili na kwa ajili ya watu wengine )

nikasema:unamaanisha nini ?

akasema :omba Mungo akutunze kotoka uovu , dhambi,tamaa na dhambi yoyote unapamaba nayo na sema

samahani Mungu kwa ajili hiki na hicho na amani katika samaha yako kamili .pia omba kwa ajili mambo ya kimwili kama masomo au kazi .mahitaji ya kimwili na kwa ajili watu wengine kama familia yako (Baba ,mama,wazangu ,ndugu.... pia mtu yeyote alikusumbua kumwombeaa .

Nikasema :nimwobee ,naweza kuomba dua juu yake .

Akasema (akitabasamu):hapana ,omba Mungu ambadilishe kwani njia bora kumwondoa adui ni awe rafiki .

Omba Mungu akupe hakima  kushughulikia naye na Mungu atawaokoa wewe na yeye kotoka uovu kwani  bindamu ni maskini .lakini shetani anamfanya bindamu awe adui kwa ndugu . tunaomba Mungu atuokoe kutoka kazi ya shatani .unaweza kuanza sala sasa kwa maneno ambayo tunayazungumzia

Nikasema :  vipi ?

Akasema :omba maneno kama hayo kila siku “je Mungu unanipenda  ,kweli, na nina ghambi na  najisi ?! watu hawajui labda  kila kitu kwangu  lakini

Mungu anajua dhambi ambazo zilikuwa kama ulevi .je unanikubali inagawa sijajua kuziancha ,ninataka kuacha kila dhambi lakini mini ni dhaifu ,kila mara najaribu naanguka nisaidie na kunipa nguvu , siye Mungu ni Baba yangu . Nimekumisi Baba , je hujanimisi ? Mungu njoo kwangu na unioneshe upendo wako niambie unanipenda zaidi ya upendo wa Baba yangu ,mama yangu na marafiki zangu . njoo uwe Baba yangu ,mama yangu ,rafiki yangu .jitambulisha Mungu , inatosha mawazo ambayo yaliyosabebisha hufu kwangu na yamenifanya chini ya utawala wa shetani na dhambi . Inaonekana unanipenda wala una huzuni kwa sababu yangu lakini huzuni ni kwa ajili yangu . kwa ajili mwanawe ambaye anatumwa na shetani ,kweli Mungu kuishi bila wewe ni utumwa na hufu . nirejee hapana nimesharejea . ninakurajia kuhafidhisha katika kifueni pako. Mungu usiniruhusu kurudi kwa dhambi .kama nikiwa dhaifu nifanye kurejea kwako kwa sababu utaniponya sitaki kuwa na hufuna au kukata tamaa au kuihisi kama hamna faida , nipe matumaini ya kuishi nawe hata nikifa wakati napogomabana na hatia na bora zaidi kukata tamaa , nisaidie kujua nimjibuje Shetani na nitumie upanga wa roho ambao ni neno lako , kwani mimi ni mjinga na hata sijui chochote nielezee , wewe ni anayenijali kutoka sasa kwa milele , naamini utakuwa nami hapa siku zote za maisha yangu na utanichukua mbinguni , Baba yangu na mpenzi wangu na maisha yangu yote " anza sasa na sema unazihisi .

Nikasema :sasa!! Kwa kweli sujui kusali .sikuzoea kuomba kama hivyo . nikiomba ninaweza kusoma maneno marufu lakini kama hivyo ni ngumu sana .

Akasema:anza na utaelimishwa na kweli uisiposema maneno yako kama hali yako ,sio maneno marufu , basi usingoje jibu !!

Nikasema : inawezekanaza kukosea na Mungu atakasirika zaidi .

Akasema ( kwa tabasimu ):kwanza kama tunazungumza hakasirika lakini anakasirika kutoka shetani ambaye anakushinda ,pili maneneo yoyote utayoyamwaambia Mungu atafurahi sana kama sala ya watakatifu .

Nikasema :samahani Baba yangu maneno yako ni mapya na megeni ,sala yangu ambayo ina dhambi na mbaya itamfurahisha kama sala ya watakatifu !!

Akasema :Baba ana wana  wengi , kijana mmoja mdogo  bado anajifunza maneno atafurahi  nani na atasikia nani hata akisoma maneno bure !

nikasema :unanishinda Baba yangu una mifano na majibu kwa kila kitu .

akasema :Munguni Baba anapenda zaidi kuliko Baba yeyote .

BWANA wadhani bora zaidi kwamba sala fupi na inaambiwa kwa njia iliyoridiwa kila mara mpaka upenda tunaweza kuzungomzo na Munguuendelea na upanda nyingeni kwa ufupi tunahazari mishale ambayo aduhi inapata ilituumiza wakati ya sala St .Yohana kasian

Baba inawezekana awe mgomu kwa mwana wake kwa hivyo Mungu anasema upendo wake kama upendo wa mamabila zaidi tu . hata Baba na mama wakiniacha ,Mungu ananizungushwa mikono .

pia,yeye ni kama rafiki zaidi  kuliko ndugo .

Mungu  anaweza kutendea kama Baba akiwa Baba mkali  atakuwa kama mama .

ikiwa mama mkali  na hajali pia mama anwezea kutendea kama rafiki

nikasema :kweli Baba yangu !

akasema :kweli mwanangu ,imeandikwa (na hukujangwani ,ulipoona alivyokuchukua BWANA,Munguwako , kama mtu amchukuavyo mwanawe,njia yote mliyoiendea,hata mkafikilia mahali  hapa (Kumbukumbu la Torati 1:31) ) pia (Mfano wa mtu ambaye mama yake amefariji, ndivyo nitakavyowafariji ninyi ; nanyi mtafarijiwa katika Yerusalemu (Isaya 66:13))

pia (Nami nawaambia ninyi rafiki zangu ,msiwaogope hao wauuao mwili ,kisha baada ya hayo hawana  wawezalo kutenda zaidi .(luka 12:4)

nikasema :maneno kama hii wapi Baba yangu ?kwanini hatusikiliza katika azaa ?kwa nini Mtumwa wa Kristo yeyoto hatusome wake katika muda ya ujana na tunahisia usisifu na kukataa kota Munguna watu hata nafsi wangu!!

Akasema :Mungu anawatuma wafanya wema kama sura yake na mfumo wake , haya mwanangu  mwomba Mwangu .

Nikasema : ukisita nisome ,Mungo nina dhambi na sijui kuomba . natakwa kukwambia mimefurahi kusikia maneno ya leo , unanipenda ingawa nina dhambi Mungu unaweza kunibadilisha na kuniponya.sijui kufanya kitu lakini nitakuja kwako na kuomba msamaha yako .nina hufo kutoka kuanguka tena ,lakini kama Baba yangu akisema nikianguka nitasimama tena na sitakata tamaa .Mungun nifundishe jinsi navyoomba na kukaa nayo daima ,umenitunza kutoka kwa shitani na dhambi zangu .

Na umenippa uhuru wangu kotoka ada zangu ambazo zilikuwa kama ulevi . sina mtu yeyote Mungu,Amina .

Akasema :hii ni mfunzo wa pili ambao utafanya kila siku mpaka nikuone usiku ujao. kila siku Mungu omba maneno kama hayo asubuhi na jioni .sala ni jambo ambalo linanibadilisha na kunisaidia kutubu dhambi .Mar Isaac akasema( usifikirii kama una mlango mwigine kwa toba bada ya kusali . umedanganyiwana shatani .

Mfunzo wa tatu. Unazungumza na Mungu kuhusu kila kitu unakihisia katika kila wakati. Unapotembea ,upo Kazini,upo bostani,upo shuleni, upo kwenye daladala , kitu kilichopo moyoni mwako kiseme . Mfanye rafiki yako

Wakati Mungu anapokaa nawe , shetani ataogopa wewe , wakati Mungu anapokuwa nawe na mnaongeana sana .kwa hivyo watakatifu waliomba kila wakati bila ya kusimamisha na kurudia jina la Yasio hata wakati wa Kulala. Kwa hivyo shaitani wanawahufia .

Nikasema :kweli Baba yangu ninapumzika baadaye kuomba, Mungu akipenda nitaomba kila siku kwani sala ni rahisi na nzuri sana.

Nitajaribu kuomba kazini njaini na kila wakati. Mtu yeyote akiweza kuongea na Mungu ana hafanyi yaani ni hastahili neema ya Mungu .

Akasema :tuna muhtasari wa maneno tuliyoyazungumzia .

**dalili ya kwanza kuwa kristo anawapenda wenye dhambi ni maneno ya Biblia takatifu.

* siri ya kubadilika na Kukubali upendo wa Mungu uhuru wake kutoka utawala wa shetani ni aya ya( Warumi 5: 8 )

Bali Mungu ameonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.

* Mafunzo

1 aya kila siku kwa wiki moja, wiki mbili aya mbili, wiki tatu sehemu ya mlengo na wiki nne nusu ya mlengo mwaka

2 sala kila siku dakika moja

Kwa muda wiki moja halafu dakika mbili kwa muda wiki mbili na dakika tano kwa muda miezi mitatu , pia usiongeze wala usipungeze. mwombe Mungu akufundishe njia na akupe amani ya kukubali na kusamahe .

3_ ongea na Mungu wakati wote , kazini barabarani ,unapolala , au hata unapoamka .

Salama mwanangu, tutakamilisha wiki ijayo dalili za Upenda wa Kiresto kwa wanao kufanya dhinaa i. Anza kufanya hatua za vitendo. Kila wiki tunakutana tunachukua hatua mpya (au soma sehemu ifuatayo) mwanzo hautoshi lakini ni muhimu mwendelezo na sabira .

Paule mtume anasema (bali mgeuzweni kwa kufanya upya nia zenu,mabadiliko ya tabia huanzakubadilisha akili ,kufikiri na kosoma ni njia muhimu zaidi kwa kulisha akili na kubadilishe .bible inasema

(Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa )kutojua husabibisha uharibifu Kama dhambi pia . tunatumani Kwamba masomo haya bure au kwa thamani rahisi ikiwezekana kwa yafikie kila mtu mkristo

Nafurahi kushirikaina katika onisho hili :

Kwanza :sala .sala ni muhimu zaidi inafanya kazi koliko zaidi kuuleza au kufikiri , tuombee pamoja na asubuhi njema .

Pili :kwa kusambaza , unaweza kutusadia kwamba mfululizo huu ufikie makanisa na huduma ni jambo muhimu sana hasa katika miji na mahali ambapo bila makanisa .

Kwa kupata kikundi kingine PDF kupitia tovuti hii

**mbade2.com**

au sikia sehemu imerekodiwa kwa sauti

**soundcloud.com/mbade2**